

HALI YA LUGHA INAYOTUMIWA KATIKA MATANGAZO YA KIBIASHARA NCHINI
KENYA

Harriet K. Ibala
Chuo Kikuu cha Moi

Ikisiri

Makala hii itatalii matangazo mbalimbali ya kibiashara yanayotumia lugha ya Kiswahili katika vyombo vya habari, magazeti na mabango ya kibiashara nchini Kenya. Baadhi ya masuala yatakayochunguzwa ni pamoja na usanifu wa lugha inayotumiwa, hadhira inayolengwa na lengo hasa la kuwa na mawasiliano katika matangazo haya. Makala hii itachanganua aina ya lugha inayotumiwa katika miktadha mbalimbali na jinsi na sababu ya lugha kubadilika katika matangazo mbalimbali. Zaidi ya hayo, makala itatalii athari za lugha inayotumiwa katika matangazo haya kwa umma, na kutoa mapendekezo kuhusu mbinu mwafaka zinazoweza kutumiwa katika matangazo ya kibiashara huku jamii ikipata faida kutokana na matangazo haya kama njia moja ya kutumia lugha na kuleta maendeleo katika jamii.